

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA**  
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Maswa)

Telegrams: "MSW"

Telephone: + 028 2750271

Fax: + 028 2750376

E-mail: [ded@maswadc.go.tz](mailto:ded@maswadc.go.tz)



S.L.P 170,  
MASWA,  
SIMIYU.

Kumb.Na.MDC/ADM/10/30.VOL.I/62

24 Machi,2021

## **YAH: TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II – NAFASI 1**

Halmashauri ya Wilaya ya Maswa kupitia kibali cha ajira mbadala **Kumb. Na.FA.170/533/01”B”/53** cha tarehe **16 Februari 2021**, kilichotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina Tangaza nafasi wazi moja [1] ya Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la II.

### **1.0. Sifa za Mwombaji:-**

- Wahitimu wa kidato cha nne au sita wenye cheti cha Utunzaji Kumbukumbu [NTA Level 5] katika mojawapo ya fani za Afya, Masjala, na Aridhi.

### **2.0. MAJUKUMU YA KAZI**

- (i) Kutafuta kumbukumbu /Nyarakaa/Mafaili yanayohitajiwa na wasomaji
- (ii) Kudhibiti upokeaji, uandikishaji wa kumbukumbu au nyaraka na utoaji wa nyaraka.
- (iii) Kuchambua, kuorodhesha na kupanga kumbukumbu au nyaraka katika makundi kulingana na Somo husika [Classification and boxing] kwa ajili ya matumizi ya ofisi.
- (iv) Kuweka/kupanga kumbukumbu na nyaraka mbalimbali katika mafaili
- (v) Kuweka /kupanga kumbukumbu/nyaraka katika reki [file racks/cabinet] katika masjala/vyumba vya kuhifadhia kumbukumbu.
- (vi) Kuweka kumbukumbu [barua,nyaraka nk.] katika mafaili.
- (vii) kushughulikia maombi ya kumbukumbu na nyaraka kutoka Taasisi za Serikali.
- (viii) Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa.

### **3.0. MASHARTI YA JUMLA**

- Awe raia wa Tanzania.
- Awe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45

- Waombaji waambatanishe na nakala za cheti cha kuzaliwa, vyeti vya kuhitimu mafunzo ya Mtunza Kumbukumbu na vyeti vya kidato cha nne vilivyodhibitishwa na Wakili au Mahakama.
- Muombaji ambatanishe picha mbili [2] ndogo ya rangi [passport size] ya hivi karibuni
- Testimonials, Provisional results, Statement of results na hati za matokeo ya kidato cha nne na sita [form VI and form IV result slip] **HAVITAKUBALIWA**.
- Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimekaguliwa na kuthibitishwa na mamlaka husika.
- Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kwa Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

#### **4.0. NGAZI YA MSHAHARA**

**Mshahara:** Ngazi ya **TGS B** kwa mwezi.

#### **5.0. UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI**

Maombi yote yatumwe kwa:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya wilaya ya Maswa,  
S.L.P. 170,  
**MASWA –SIMIYU.**

Mwisho wa kupokea maombi ni **tarehe 07.04.2021 saa 9.30 alasiri.**

**NB:**

Tangazo hili linapatikana katika Tovuti ya Halmashauri [www.maswadc.go.tz](http://www.maswadc.go.tz) Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira [www.ajira.go.tz](http://www.ajira.go.tz) na katika mbao za matangazo za Halmashauri na Mkoa wa Simiyu.



Dr.Frederick D.Sagamiko  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W),**  
**HALMASHAURI YA WILAYA**  
**MASWA,**

*MKURUGENZI MTENDAJI  
 HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA*